# DCEA yateketeza ekari 291.2 Mara

**Na Hamisi Miraji,**

KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, amesema kilimo cha bangi katika Mkoa wa Mara kimepungua kwa takribani asilimia 80 kutokana na operesheni endelevu zinazotekelezwa na Serikali katika kukabiliana na uzalishaji wa dawa za kulevya.

Hayo aliyasema Julai 24, 2026, baada ya kuhitimisha operesheni maalumu zilizofanyika katika Wilaya za Tarime na Rorya, Lyimo.

Alisema, operesheni hizo zimefanikisha kuteketezwa kwa mashamba ya bangi yenye ukubwa wa ekari 291.2.

Lakini pia, kukamatwa kwa magunia 15 ya bangi kavu pamoja na pikipiki nne zilizokuwa zikitumika katika shughuli hizo haramu.

Aidha, watu wawili walikamatwa huku uchunguzi ukiendelea kuwabaini na kuwakamata washirika wengine waliohusika katika mtandao huo.

Alisema, mafanikio hayo yanathibitisha ufanisi wa operesheni za Serikali, akibainisha kuwa mwaka 2024 zaidi ya ekari 3,500 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika Mkoa wa Mara.

Hatua hiyo, imechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza uzalishaji wa bangi na kudhoofisha mtandao wa kilimo hicho katika maeneo yaliyokuwa yakiathirika zaidi.

"Matokeo haya yanaonesha kuwa juhudi za Serikali zinaendelea kuzaa matunda. Wananchi wengi wameanza kuachana na kilimo cha bangi na kuelekeza nguvu zao katika shughuli halali za uzalishaji zinazowanufaisha wao, familia zao na Taifa kwa ujumla," alisema Kamishna Jenerali Lyimo.

Kamishna Jenerali aliwataka wananchi ambao bado wanajihusisha na kilimo cha bangi kuachana na shughuli hiyo mara moja na kuwekeza katika kilimo halali cha mazao ya chakula na biashara.

Aliwahimiza kuendelea kushirikiana na DCEA na vyombo vingine vya dola kwa kutoa taarifa za siri kuhusu watu wanaojihusisha na uzalishaji, usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya.

Hata hivyo alisisitiza kuwa, DCEA itaendelea kuimarisha operesheni, doria na uchunguzi wa kina katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wote watakaobainika kujihusisha na makosa ya dawa za kulevya.

Kwa upande wake, Afisa Tarafa wa Nchaje, Stephano Peter Kiabaroti, alisema uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan umeongeza uwezo wa DCEA kutekeleza operesheni zenye matokeo makubwa katika kudhibiti na kutokomeza kilimo cha bangi.

Alisema, wananchi wengi waliokuwa wakitegemea kilimo hicho sasa wamehamia katika uzalishaji halali wa mazao ya chakula na biashara pamoja na shughuli za ufugaji, hatua ambayo imeanza kuleta manufaa ya kiuchumi kwa familia na jamii kwa ujumla.

Naye Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Rozana, Kurwa Robert, alisema kabla ya operesheni hizo matumizi na biashara ya bangi vilichochea ongezeko la vitendo vya uhalifu, huku baadhi ya vijana wakijihusisha na makundi ya uhalifu na kujichukulia sheria mkononi.

Alisema, baada ya DCEA kuimarisha operesheni za kuteketeza mashamba ya bangi, hali ya usalama imeimarika kwa kiasi kikubwa na wananchi wameanza kurejea katika shughuli zao za kila siku kwa utulivu.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nkerege, Joseph Mwita Ryoba, alisema kijiji hicho kilikuwa miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi na kilimo cha bangi, ambapo mwaka 2024 zaidi ya ekari 3,000 ziliteketezwa katika operesheni za Serikali.

Alisema, kwa sasa wananchi wengi wameachana na kilimo hicho na kuelekeza nguvu zao katika shughuli halali za uzalishaji, jambo linaloonesha kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu madhara ya dawa za kulevya na umuhimu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

## Umuhimu upandaji miti ya vivuli, matunda wasisitizwa

**Na Mwandishi Wetu,**

WATANZANIA, viongozi, pamoja na sekta mbalimbali zimeombwa kuhakikisha zinaona umuhimu wa kupanda miti ya vivuli na matunda.

Wito huo ulitolewa Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na mmoja wa viongozi aliyekuwa mgombea wa ubunge viti maalum Taifa mwaka 2025 kupitia Umoja wa Wazazi Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni mfanyabiashara Olivia Chagula.

Alisema hayo wakati wa kongamano la upandaji miti katika maeneo mbalimbali kongamano lililoandaliwa na Taasisi ya Samialism inayojihusisha na masuala mbalimbali ya kitaifa chini ya mwenyekiti wake Taifa, Charles Sabiniani (Lowassa).

Alisema, viongozi wote kwa kushirikiana na Serikali wanatakiwa kuona umuhimu wa kuwaelekeza watoto wao na vijana wote wa umuhimu wa kupanda miti na kuweka mazingira katika hali mzuri.

"Unajua kuna jambo muhimu sana ambalo tunatakiwa kulijua kwamba hii miti inatusaidia katika mambo mbalimbali kupata matunda, vivuli, kuzuia mmomonyoko wa ardhi na mambo mengine mengi hivyo kuna haja ya kuhakikisha jambo hili linapewa uzito zaidi kwa vijana wetu na Watanzania kwa ujumla, lakini pia na kujua kwamba tunamuunga mkono Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan"; alisema Olivia.

Mwenyekiti Lowassa, alisema kuwa zoezi la kupanda miti halitaishia hapo, bali taasisi yake kwa kushirikiana na wadau wengine wataendelea kupanda miti hiyo maeneo mbalimbali lengo likiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia

Katika kongamano hilo wadau mbalimbali wa mazingira waliudhuria ambapo Mwanadiplomasia na Mratibu wa Makongamano ya Vijana, Omary Abdall Punzi alisema yeye akiwa kiongozi anaamini mkusanyiko wa viongozi mbalimbali waliokusanyika na kujadili masuala ya Kitaifa utaleta tija kwa Taifa.




**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, akisistiza jambo wakati wa kufunga mafunzo elekezi kwa wakuu wa taasisi yaliyoandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Kibaha, Pwani hivi karibuni. (Na Mpigapicha Wetu)**

# Mapato Airtel Africa yafikia dola bil. 1.85

**Na Mwandishi Wetu,**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Airtel Africa, imeanza mwaka mpya wa fedha wa 2026/27 kwa mafanikio makubwa, baada ya kuongeza mapato kwa asilimia 31 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026/27, yakichochewa na kasi kubwa ya matumizi ya intaneti na huduma za kifedha kwa njia ya matokeo hayo.

Mtendaji Mkuu wa Airtel Africa, Sunil Taldar, alisema mapato ya kampuni hiyo inayofanya kazi katika nchi 14 barani Afrika, ikiwemo Tanzania, yalifikia dola bilioni 1.853 za Marekani kwa robo mwaka iliyoishia Juni 30, 2026, ikilinganishwa na dola bilioni 1.415 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Faida baada ya kodi ilipaa kwa asilimia 27 na kufikia dola milioni 198. Kwa kuzingatia viwango vya fedha visivyobadilika (constant currency), mapato ya kampuni yalikua kwa asilimia 21.1, yakionyesha ukuaji thabiti katika huduma za sauti, intaneti na Airtel Money.

Ripoti hiyo inaonyesha ukuaji mkubwa katika maeneo yote makuu ya kibiashara ambapo soko la Nigeria liliongoza kwa kukua kwa asilimia 29.8, likifuatiwa na ukanda wa Afrika ya Kati na Magharibi inayozungumza Kifaransa (Francophone Africa) uliokua kwa asilimia 18, huku ukanda wa Afrika Mashariki ukikua kwa asilimia 17.8.

Ukuaji huo unachochewa na ongezeko kubwa la wateja ambapo katika nchi zote 14, jumla ya wateja wa Airtel iliongezeka kwa asilimia 11.6 hadi kufikia milioni 189.Ripoti hiyo inaonyesha kuwa asilimia 51 ya wateja wote wa kampuni hiyo sasa wanatumia simu janja (smartphones).

Hali hiyo imesababisha idadi ya wateja wa intaneti kuongezeka kwa asilimia 15.5 hadi kufikia milioni 87.3.Kasi ya matumizi ya intaneti imeongezeka kwa kiwango kikubwa, ambapo wastani wa matumizi ya data kwa mwezi kwa kila mteja ulipaa kutoka Gigabaiti (GB) 7.8 hadi kufikia GB 10.6, na kupelekea matumizi ya intaneti (data traffic) kuongezeka kwa asilimia 56.3 ndani ya mwaka mmoja.

Upande wa huduma za kifedha, wateja wa Airtel Money waliongezeka kwa asilimia 23.3 hadi kufikia milioni 56.5.

Thamani ya miamala inayofanyika kupitia Airtel Money sasa imevuka dola bilioni 245 za Marekani kwa mwaka (ongezeko la asilimia 51.5), huku mapato ya huduma hiyo pekee yakikua kwa asilimia 38.9 na kufikia dola milioni 404.

Ili kuhimili kasi hiyo ya ukuaji na mahitaji makubwa ya wateja, Airtel Africa imewekeza kiasi cha dola milioni 389 za Marekani katika robo-mwaka hiyo kwa ajili ya kupanua miundombinu yake.

Airtel Africa pia ilifanikiwa kujenga minara na vituo vipya vya mawasiliano zaidi ya 920, ikiwa ni idadi kubwa zaidi kuwahi kujengwa katika robo ya kwanza ya mwaka katika historia ya kampuni hiyo, pamoja na kutandaza mtandao wa nyaya za mawasiliano (fibre) hadi urefu wa kilomita 82,100 ili kuimarisha upatikanaji wa huduma bora.